Sauti ya Siti

Toleo Na. 40 | ISSN 0856 - 230 X | Novemba, 2023

Rushwa ya Ngono ndani ya Vyombo vya Habari

Uk. 2 "Sikuruhusu Ngono Itumike Kama Kipimo cha Kazi Yangu"

Uk. 5 Rushwa ya ngono: Uhalifu uliokithiri dhidi ya Wanahabari Wanawake vijana

Uk. 13 Rushwa ya Ngono Inavyochochea Wanahabari Wanawake Kuwa Tegemezi Kiuchumi

TAMWA

Sauti ya Siti

Mkurugenzi Mtendaji- TAMWA
Dkt. Rose Reuben

Mhariri Mkuu:
Dkt. Ananilea Nkya

Mhariri Msaidizi:
Edina Salila

Usanifu
Gurnam Ajit

Mawasiliano:

Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA)
S. L. P 8981, Sinza - Mori,
Dar es Salaam

B/Pepe: tamwa@tamwa.org

Zanzibar Office:
S. L. P 741, Tunguu,
Zanzibar, Tanzania
Simu: +255 773 747 252
B/Pepe: tamwazanzibar@tamwa.org

Tovuti: www.tamwa.org

YALIYOMO

TAHARIRI 1

"Sikuruhusu ngono itumike kama kipimo Cha kazi yangu" 2

Rushwa ya ngono: Uhalifu uliokithiri dhidi ya wanahabari wanawake vijana 5

Rushwa ya ngono kwa wanahabari wanawake iko maeneo matatu 8

Fikiria hatma ya uandishi wa habari Afrika bila wanawake 10

Rushwa ya ngono inavyochochea wanahabari wanawake kuwa tegemezi kiuchumi 13

Rushwa ya ngono kwenye vyombo vya habari: Safari bado ndefu 16

'Rushwa ya ngono inatutesa wanahabari tunaojitolea' 18

"Najuta kukubali rushwa ya ngono" 20

"Nilikua na wakati mgumu sana" 22

Usiri unaendeleza rushwa ya ngono 24

TAHARIRI

Vyombo vya habari viwe mfano kukomesha rushwa ya ngono

MWAKA 2020, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilifanya utafiti katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kuhusu rushwa ya ngono katika vyuo vikuu.

Zaidi ya asilimia 50 ya waliohojiwa walieleza kuwepo kwa rushwa ya ngono vyuoni.

Mwaka 2021, Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kwa kushirikiana Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T), nacho kikafanya tathmini ya awali ya mradi wa kutoa elimu na mafunzo kuhusu rushwa ya ngono katika vyumba vya habari vya Dar es Salaam.

Tathmini hiyo ilihusisha vyombo 20 na wanahabari 25 wakiwamo wandishi wa habari wasio waajiriwa, walio katika mafunzo kwa vitendo na wahariri wa televisheni, redio, magazeti, vyombo vya kijamii na vyombo vya habari vya kidijiti.

Kimsingi, ililenga kuangalia hali ya rushwa ya ngono kwa wanahabari katika vyumba vya habari na namna ya kuikabili ili isizidi kuwaathiri na taaluma yao tangu wakiwa vyuoni na katika mafunzo kwa vitendo.

Ripoti ya tathmini ilisema asilimia 48 ya waandishi wa habari wasio na ajira rasmi wamewahi kukumbwa na visa vinavyohusu madai ya rushwa ya ngono katika vyumba vya habari. Asilimia 52 ya waliohojiwa, walikaa kimya.

Ilibainika kuwa, waathirika wakubwa wa rushwa hiyo katika vyumba vya habari ni waandishi wahabari wanawake wanaolipwa kwa idadi ya ripoti au makala wanazoandika na wanafunzi walio katika mafunzo kwa vitendo.

Sauti Ya Siti tunasema, matokeo hayo yanaonesha dhahiri tatizo la rushwa ya ngono katika vyumba vya habari, limejificha katika ukimya wa hatari.

Wandishi wa habari ambao wanapaswa kuwa sauti ya wasio na sauti, nao wanafanya kosa na kulikalia kimya uovu huu unaoharibu heshima ya vyombo vya habari utu wa binadamu na kudidimiza maendeleo ya nchi yetu.

Sauti ya Siti tunasema, ukimya unazidi kutoa fursa kwa watu wenye mamlaka wanaojiuhusisha na rushwa ya ngono kujificha na kuendeleza uhalifu huu bila hofu kama kwamba wana haki ya kutenda uovu huo.

Hapana shaka kuwa, ukimya katika rushwa ya ngono unatokana na waathirika kuhofia kutosikilizwa na wanachukuliwa kama ndio wakosaji, wasababishi na wanajengewa kinyongo na hata kuchafuliwa sifa kila waendapo badala ya kusaidiwa ili sheria ichukue mkondo wake dhidi ya watenda uhalifu huo.Kimsingi, ukimya ndio kosa kubwa la kijamii katika vita hii.

Ikumbukwe kuwa, Kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 kinasema, mtu anayetumia mamlaka yake ya utekelezaji majukumu yake kuomba au kutoa upendeleo wa kingono, kama kigezo cha kutoa ajira, kupandisha cheo, kutoa haki au huduma, anakuwa anatenda kosa la kudai rushwa ya ngono.

Tunapinga rushwa ya ngono na tunapaza sauti zetu kwa sababu tunafahamu ina madhara kwa waandishi wa habari, wanawake kwa sababu ingawa ni wanawake wengi wanaosomea taaluma ya habari ni wachache wanaoonekana kwenye vyombo vya habari.

Kadhalika rushwa ya ngono ina madhara kwa jamii na taifa kwa sababu wanawake wanasoma uandishi wa habari na wale wanaolipwa kwa idadi ya taarifa au makala zilizochapishwa kutokutangazwa au kutokutumika hata kama zimeandaliwa kwa ubora unaotakiwa.

Matokeo yake baadhi ya vyombo vya habari kuajiri wanahabari wasio na sifa na hivyo, vyenyewe kujipotezea heshima mbele ya jamii.

Ndio maana tunasema, vyombo vya habari viwe mfano bora katika kukomesha uovu huu kwenye vyombo hivyo na kwa jamii nzima. Rushwa ya ngono itadhibitiwa endapo wanahabari watavunja ukimya hata linapotokea miongoni mwao maana wema huanzia nyumbani.

Kama wanajamii wengine, wanahabari wawe tayari kutoa ushahidi ili wahusika 'wakione cha mtema kuni' mbele ya sheria.

Ndio sababu sisi wamiliki wa Sauti Ya Siti tunavitaka vyuo vyote vikiwamo vya uandishi wa habari na vianzishe, visimamie na viendeleze madawati makini ya kushughulikia masuala ya haki na usawa wa jinsia.

Muhimu zaidi ili kumaliza rushwa hiyo vyuoni na katika vyumba vya habari, nguvu za pamoja ya vyombo vya habari kwa ujumla wake, wanahabari wanawake na wanaume,vyombo vya serikali na wote wenye mapenzi mema zinahitajika ili vyombo vya habari viweze kutoa mchango wake kikamilifu kwa maendeleo ya taifa letu..

“Sikuruhusu ngono itumike kama kipimo cha kazi yangu”

Na Elizabeth Edward

Mmoja wa wahanga wa rushwa ya ngono ndani ya vyombo vya habari (jina limehifadhiwa) (Picha na TAMWA)

“Isingekuwa ujasiri na kujiamini huenda ningekuwa miongoni mwa waathirika wa rushwa ya ngono”, anasema Devotha Kihwelo mwandishi wa habari mwanamke hapa nchini.

Devotha ambaye amefanya kazi ya uandishi kwa zaidi ya miaka kumi amewahi kujiuzulu kazi katika vyombo vinne baada ya kukataa rushwa ya ngono. Lakini pia suala hilo likatumiwa kama kipimo cha utendaji kazi wake na hatimaye akaishia kutopangiwa kazi.

“Binafsi najiona kama nyani mzee nimekwepa mishale mingi kufika hapa nilipo leo hadi naweza kuzungumzia suala hili,”.

Pengine ujasiri wa Devotha unatokana na juhudi ambazo zimekuwa zikifanywa na Mtandao wa Wanawake dhidi ya Rushwa ya ngono ambao tangu mwaka 2000 umekuwa ukiendesha harakati za kupinga rushwa ya ngono kwa kauli mbiu “vunja Ukimya dhidi ya Rushwa ya Ngono”.

Rushwa ya ngono ni kosa kisheria .kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kililenga kuwawajibisha wenye mamlaka kufuata miiko ya uongozi katika nyadhifa walizopewa dhamana ya kuzisimamia. Hata hivyo serikali inakusudia kufanyia maboresho kwa kuongeza kifungu 25(2).

Wanaharakati wa haki za wanawake, wasichana na watoto wanasema kifungu hicho kinachopendekezwa kuongezwa kinaondoa maana ya kifungu cha 25 kwa sababu kinasema mtu atakayemsababishia mtu mwenye mamlaka kutenda kosa la rushwa ya ngono atahukumiwa kulipa faini ya shilingi milioni mbili hadi 10 au kifungo cha hadi miaka mitano jela.

Licha ya kwamba tatizo hili linazidi kuota mizizi ni nadra kukuta wahanga wanaeleza wanayokabiliana nayo hali inayosababisha vitendo hivi kuendelea kuathiri kundi kubwa wengi wakiwa wanawake.

Utafiti uliofanywa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) uliolenga kuangalia rushwa ya ngono kwenye vyombo vya habari, ulibaini kwamba waathirika wamekuwa na vigugumizi wanapotakiwa kuzungumzia suala hilo. » Uk 3

Uk 2

“ Sikuruhuru ngono ....”

Ripoti hiyo ilionyesha asilimia 52 ya wahojiwa hawakuwa wazi kusema kuhusu hilo licha ya kukiri kwamba rushwa ya ngono ipo kwenye vyombo vya habari.

Safari ya miaka 10 ya Devotha kwenye tasnia ya habari haikuwa rahisi kwani ulifika wakati aliamua kujiweka kando na fani hiyo kutokana na mwendelezo wa matukio aliyokuwa akikutana nayo katika sehemu alizofanyia kazi kwa sababu tu ya kukataa kutoa rushwa ya ngono.

Binti huyu alianza kupitia magumu tangu akiwa katika mafunzo kwa vitendo ambako alikutana na mhariri aliyekuwa akimtaka kimapenzi kwa ahadi ya kumpatia kazi ambazo zingemuwezesha kupata fedha.

“Kwa mtu ambaye hajapitia haya anaweza asielewe ukubwa wa tatizo hili, binafsi sehemu kubwa ya maisha yangu ya uandishi ya habari imegubikwa na aina hii ya rushwa lakini hata siku moja sikuruhusu hilo lifanikiwe”,anasema Devothat na kuongeza:.

“Nakumbuka baada ya kumaliza chuo nilienda kwenye gazeti moja kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo, nilipokelewa vizuri nikaanza kujifunza pale”.

Devota anasema “ikafika muda mhariri wangu akawa ananituma kwenye kazi ambazo zina hela, nilikuwa naenda kuzifanya na kuleta stori kama inavyotakiwa. Sikuwa nafahamu kwamba mwenzangu ana mawazo yake na hiyo ndiyo ilikuwa njia yake ya kunifikia,”

Iliendelea hivyo hadi alipomaliza mafunzo kwa vitendo na hatimaye akapata nafasi ya kuendelea kufanya kazi kwenye gazeti hilo hapo ndipo mambo yalipozidi kupamba moto

Baada ya muda kupita hatimaye mhariri huyo akavunja ukimya na kumueleza wazi kwamba anataka kuwa na uhusiano naye wa kimapenzi na hiyo ndiyo sababu alikuwa akimtengenezea michongo ya kupata fedha.

“Ilibidi nimuulize mara mbili mbili ili nimuelewe alichokuwa akimaanisha, bila hiyana akasema ananitaka kimapenzi, nilijaribu kumwambia kwa uwazi kwamba hilo si lililonipeleka hapo kazini lakini hakuelewa. Aliendelea kushililia msimamo wake kwa muda mrefu na alipoona sieleweki akanibadilikia.

“Hapo ndiyo nikaanza kupata machungu, akawa hanipi tena kazi na hata zile ninazohangaika kuzipata mwenyewe akawa hatoi stori zangu. Kwa maisha ya uandishi hakuna kitu kinaumiza kama mwandishi uhangaike kuitafuta stori halafu mtu aamue tu kwamba haitoki bila kukupa sababu,”anasema.

Hilo halikumkatisha tamaa akatafuta njia nyingine ya kuhakikisha stori zake zinatoka, ikawa inamlazimu kuwa anatengeneza stori maalum ambazo zinatoka siku ambayo mhariri huyo hayupo.

Njia hiyo ilimsaidia kwa muda mfupi kabla ya kuanza kusikia habari za uzushi kumhusu tena akihakikishiwa kwamba zinatoka kwa yule mhariri aliyekata kujihusisha naye kimapenzi.

Baada ya kuvumilia hayo kwa muda mrefu akafikia uamuzi wa kuacha kazi katika gazeti hilo na kutafuta fursa kwenye gazeti lingine akiamini huko mambo yatakuwa tofauti.

Hakuwa na tofauti sana na mawazo yake, alipofika kwenye hilo gazeti lingine mambo yalikuwa tofauti kabisa na kule alikotoka, alifanya kazi kwa jitihada kubwa akiamini kwamba yuko mahali sahihi.

“Nilipofika huko nikiwa mwandishi wa habari za michezo nikakuta safari za nje kwa waandishi ni jambo kubwa mno kiasi kwamba watu walikuwa wanachukulia hiyo kama njia moja wapo ya kuwapata wanawake.

“Haikuchua muda mrefu akanifuata mtu kuniambia kwamba yuko tayari kunifanyia mpango na mimi niwe naenda safari za nje endapo nitakubali kuwa na uhusiano naye wa kimapenzi, nilishangazwa na hili nikajiuliza hivi kwani uwezo una nafasi gani katika kufanya maamuzi yanayohusu kazi, sikupata majibu,”.

Uk 4

TAMWA ilipoungana na TGNP katika kusherehekea miaka 30 ya taasisi hiyo yaliyoambatana na Tamasha La Jinsia la 15 lililofanyika Novemba 7-10, 2023 katika viwanja ya TGNP, jijini Dar Es Salaaam.

“Sikuruhusu ngono itumike kama kipimo cha kazi yangu”

Kwa mara nyingine maisha yake yakawa ya kuzongwa zongwa na mtu huyo ambaye licha ya kutokuwa kiongozi wake ila alikuwa miongoni mwa wenye ushawishi kwa watu wanaofanya maamuzi, hilo likaanza kumpa wakati mgumu.

Ikamlazimu kufikiria kwa kina kuhusu hatima ya maisha yake ndani ya vyumba vya habari ndipo alipofanya uamuzi wa kuacha kazi hiyo ili kutafuta ujuzi mwingine.

“Nilizungumza na mwenza wangu nikamwambia nahitaji fedha nisome kitu kingine, akaridhia na kweli akanipatia nikaenda kusoma kozi ya graphics design. Nilipomaliza kozi hiyo haikunichukua muda nikapata kazi kwenye blog ambayo kwa uhalisia ni kama tuliianzisha mimi na yule mwenyewe.

“Tulianza vizuri lakini baada ya muda kidogo bosi akaanza kuniletea yale mambo yaliyonifanya nikimbie kwenye magazeti, nikaona sasa maisha yangu yatakuwa na changamoto na hata kazi yenyewe sikuona haja ya kuendelea nayo kwa mara nyingine nikaacha kazi,” anasema Devotha.

Kwa kuwa bado uandishi ulikuwa ndani ya moyo wake, akaamua kutupa karata nyingine safari hii akapata nafasi redioni, akianza kutumika kama mchambuzi wa habari za michezo akiwa nje ya studio.

Kutokana na kufanya kazi hiyo kwa umahiri mkubwa msimamizi wa vipindi akavutiwa na kuonyesha nia ya kumuhitaji ajiunge moja kwa moja na redio hiyo kama mchambuzi ndani ya kipindi hicho cha michezo.

Wakati mchakato wa kufanikisha hilo ukiendelea akawa anakwenda viwanjani kwa ajili kuripoti mechi mbalimbali, haikupita muda mrefu akakutanishwa na mmiliki wa redio ambaye alikuwa mwanamke.

“Yule msimamizi wa vipindi ambaye kwangu mie ndiye alikuwa bosi akanitambulisha kwa mmiliki akimueleza kazi zangu na nia yake ya kunihitaji nipate nafasi ya kuingia kabisa studio, basi nikawa nasubiri mchakato ukamilike ili niingie kwenye mfumo.

“Haikupita muda bosi wangu akaanza kuniletea habari za kunitaka kimapenzi, nilipokataa visa vikaanza na hata ule mchakato ukaishia hapo baadaye nikaambiwa kwamba sihitajiki pale kwa kuwa sina sifa za kuingia studio. Nilijaribu kufuatilia kwa yule mama nikagundua yeye hana shida nikajua tayari mdudu ameshaingia basi nikaacha kama nilivyoacha kwingine,” anasema Devotha.

Ilipofika hatua hiyo alikata tamaa ya kuhudumu katika fani ya uandishi wa habari na kufikia uamuzi wa kuachana kabisa na taaluma hiyo na kugeukia biashara.

“Ilibidi nimuulize mara mbili mbili ili nimuelewe alichokuwa akimaanisha, bila hiyana akasema ananitaka kimapenzi, nilijaribu kumwambia kwa uwazi kwamba hilo si lililonipeleka hapo kazini lakini hakuelewa. Aliendelea kushikilia msimamo wake kwa muda mrefu na alipoona sieleweki akanibadilikia.

Kwa kuwa alikuwa na utundu kwenye fani ya ususi, aliamua kufungua saluni akaanza kushughulika na kuwapendezesha wanawake akiweka kando kabisa fani ya uandishi wa habari.

Baada ya kupita muda mrefu akiwa kwenye biashara hiyo, shauku yake ya uandishi wa habari ikarejea tena, akajaribu kutupa karata yake na hatimaye kwa sasa ni mwandishi wa habari anayeandika katika miongoni mwa magazeti yanayotoka kila siku.



RUSHWA YA NGONO:

Uhalifu uliokithiri dhidi ya wanahabari wanawake vijana

Na Alexander Joseph

Sera ya Jinsia katika Vyombo vya Habari ya Mwaka 2019 iliyoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania inasema, unyanyasaji uliokithiri sehemu za kazi kuwa ni pamoja na utongozaji wenye kero na masharti yanayolazimisha uhusiano wa kingono.

Wakati sera hiyo ikisema hayo, Kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 kinasema, anayebainika kutumia mamlaka ya utekelezaji majukumu yake kuomba au kutoa upendeleo wa kingono, kama kigezo cha kutoa ajira, kupandisha cheo, kutoa haki au huduma, atashitakiwa chini ya Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi.

Kwa mujibu wa kifungu hicho, mtu huyo akitiwa hatiani, anaweza kuhukumiwa faini isiyozidi Sh milioni 5, au kifungo cha miaka 20 jela, au adhabu zote kwa pamoja.

Kutokana na ukimya kuhusu janga hili lenye madhara mengi kijamii, kiafya na kiuchumi kwa taifa, Ofisa Uchechemuzi na Mawasiliano wa Chama Cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Florence Majani anasema: “Wanahabari tumekuwa wazuri sana kuandika yaliyopo kwa wengine kwa mfano, rushwa ya ngono vyuoni, hospitali na kwingine, lakini hatusemi katika vyombo vyetu tukoje… Huko nako ipo sana, lakini hatusemi…”

Uk 6

Uk 5

Rushwa ya ngono: Uhalifu uliokithiri dhidi ya Wanahabari Wanawake vijana

Sauti ya Mhanga wa Rushwa ya Ngono
Nyambuzi Nyambata (si jina halisi) ni mmoja wa wandishi wa habari wanawake walioteswa na vitendo vya rushwa ya ngono katika vyumba (vyombo) vya habari.

Anasema amefanya kazi katika kampuni moja ya vyombo vya habari inayomilikiwa na taasisi ya dini kwa miaka zaidi ya mitano kwa mfumo wa 'kujitolea'.

"Tulipotoka chuoni, tuliingia pale tukiwa wasichana sita. Kwamba tujitolee, lakini tutaajiriwa taratibu kadiri ya muda na nafasi za kazi zinavyopatikana. Lakini, ili uajiriwe lazima upendekezwe na mkuu wako (mhariri) maana ndiye anayejua utendaji wako," anasema.

Anasema siku za mwanzo yeye na mwenzake mmoja, walikuwa wakiwasilisha kazi zinazopendwa na kupongezwa, lakini kadiri walivyoongeza juhudi, nafasi ya kazi zao redioni ikawa inapungua kwa kasi huku, mhariri akiwa mkali na anayewafokea mara kwa mara huku akidhihaki kazi zao.

"Kumbe kwa nafasi hiyo, mhariri wetu alikuwa anaona kama amepewa ruksa ya ndoa za mitala; nyumbani kwake aache mke na kazini awakute 'wake zake.' Hata hivyo, tulichelewa kubaini kwa nini hali iko hivyo…" anasema.

Kwa mujibu wa Nyambuzi, mwenzake aliamua kuacha uandishi wa habari na kujikita katika biashara.

"Nikawa nashangaa maana kila mara wenzangu wanapewa safari na kazi kubwa za heshima tena zenye posho nzuri, lakini wanaporudi 'wanaleta pumba tu stori' haina kichwa wala miguu", amesema na kuongeza;

"Kila mara mimi napangiwa zamu za usiku maana kila mmoja anapenda alale nyumbani. Sikuwa najua kuwa ninaadhibiwa. Kwa kweli nilikuwa naumia sana lakini, nikajipa moyo na kuvumilia".

Anasema "mwanzoni sikuelewa lengo wala maana lakini, kila mara kupitia utani, au nilipopeleka suala langu kwa bosi huyo, maneno ya kwanza aliyokuwa akisema ni: 'Wewe si unajidai kuninyima; shauri zako

endelea kubana; utakula jeuri yako hili ni jiji (Dar es Salaam), jiongeze…"

Katika mazungumzo na ***Sauti Ya Siti*** hivi karibuni, Nyambuzi anasema awali hakuwa anatilia maanani kwani alijua ni utani tu maana 'kazi na dawa.'

Anasema "nilibaini kilichokuwa kinaendelea baada ya kugundua kuwa kumbe wenzangu walipendekezwa na kupata ajira baada ya kujitoa na kuingia katika mtego wa ngono ili waajiriwe; kwamba walikuwa 'wakimfurahisha' maana walichukiana wenyewe kwa wenyewe hadi mambo yakawa hadharani maana penzi halifichiki."

Nyambuzi anaongeza "ndipo nikagundua kwanini wenzagu walikuwa wanakula bata lakini mimi na mwenzangu licha ya juhudi na ubora wa kazi zetu, tunaishia kufokewa na kazi zetu kutupwa kapuni kumbe ni kwa kuwa tumegoma kuingia katika mtego wa rushwa ya ngono."

Anasema bahati nzuri kwake ni kwamba, kutokana na ubora wa kazi zake chache zilizoonekana, menejimenti iliamua kumwajiri bila kutegemea pendekezo la mhariri baada ya kutokea nafasi za kazi.

Katika moja ya semina zilizoandaliwa na TAMWA jijini Dar es Salaam 2022, wanahabari wengi walisema udanganyifu wa baadhi ya watendaji wenye mamlaka katika vyumba vya habari dhidi ya wandishi wanaokwenda kufanya mazoezi kwa vitendo ni janga linalowaingiza wanahabari hao katika mtego wa rushwa ya ngono ili waajiriwe au kazi zao zionekana kwa wingi na ubora.

'Wasichana wengi wanatishiwa huku wakidanganywa kuwa watapewa ajira, cheo, mshahara mkubwa na hata kupangiwa safari kubwa na zenye marupurupu makubwa mara kwa mara. Kwa watu wa broadcasting (utangazaji) wanaanza kupangiwa kazi za studio na vipindi vikubwa vikubwa," anasema Nyambuzi.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na TAMWA kwa kushirikiana na Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T) mwaka 2021, taarifa nyingi za wanafunzi wa kike wanasoma uandishi wa habari hazitumiki kutokana na kuwapo kwa rushwa hiyo hata katika baadhi ya vyombo vya habari. Uk 7

Uk 6

Rushwa ya ngono: Uhalifu Uliokithiri dhidi ya wanawake wanahabari vijana...

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk Rose Reuben anasema utafiti huo uliyofanyika Dar es Salaam ulibainisha kuwa, asilimia 48 ya waandishi wa habari wasio na ajira rasmi maarufu 'correspondent' wamewahi kukumbwa na visa vinavyohusu madai ya rushwa ya ngono katika vyombo vya habari.

Dk Rose anasema:"Asilimia 52 walikaa kimya; hawakuwa tayari kusema kuhusu rushwa hii… Nasisitiza hii ni kwa wachache tuliowafikia."

Changamoto Kubwa
Ili kushinda vita dhidi ya rushwa ya ngono katika vyumba vya habari, Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) katika Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza, Elly Makala anasema, wanahabari wana wajibu wa kuripoti kuwapo kwa madai na mazingira ya rushwa ya ngono katika vyombo vya habari ili yashughulikiwe kwa mujibu wa sheria.

"Katika kipindi nilichokuwa katika utumishi ndani ya TAKUKURU sijawahi kuona wala kusikia mwanahabari amejitokeza kutoa taarifa kuhusu vitendo vya rushwa ya ngono wanavyokutana navyo wanapotekeleza majukumu yao," anasema.

Anaongeza: "Wanapoona hayo, watoe taarifa ili tatizo hilo lishughulikiwe; wasikae kimya na kuishia kuandika ya wengine huku wao wanaumia. Uwazi na kuripoti tatizo ni silaha muhimu ya kushinda tatizo hili…"

Madhara ya Rushwa ya Ngono
Vyanzo mbalimbali vinataja madhara ya rushwa ya ngono katika vyumba vya habari kuwa ni pamoja na jamii kunyimwa haki ya kupata habari bora zaidi kutoka kwa mwandishi mwanamke aliyeombwa rushwa ya ngono na kukataa hatimaye kujengewa chuki na habari zake kutotumika.

Mkurugenzi wa shirika la kutetea la Human Life International (HLI), Kanda ya Afrika kwa nchi zinazozungmza Kiingereza, Emil Hagamu anasema rushwa ya ngono katika maeneo ya kazi huchochea utoaji mimba, magonjwa ya zinaa na msongo wa mawazo unaosababisha wengine kujiua.

Dk Rose anasema: "Wanafunzi wengi wanasoma uandishi wa habari lakini kutokana na rushwa ya ngono ni wachache sana wanaoonekana katika vyombo vya habari" na kuongeza;

"Wanapoona wanavyopambana na rushwa ya ngono tangu vyuoni, wakifika kuomba kupokelewa 'newsroom,' akienda kutafuta stori pia anakutana na rushwa ya ngono na hata akiandika habari ili itoke, baadhi ya wahariri wanataka rushwa ya ngono; wéngine wanaamua kujitoa kwenye taaluma. Hili si jambo jema," anasema.

"Tatizo hili ndilo hufanya baadhi ya vyombo vya habari kuajiri wanahabari wasio na sifa na vyenyewe kujipotezea heshima mbele ya jamii" anasema Joseph Sabinus, Mratibu wa gazeti la Habari LEO Afrika Mashariki linatolewa na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) na kuongeza;

"Yaani unakuta mtu anakwenda kwa 'source' (chanzo cha habari) akiwa hajui anakwenda kufanya au kuuliza nini, mwingine anakuwa bubu, au anauliza kitu cha ajabu na hata kuelezea kwa mhariri au kuandika, pia ni majanga."

Mwenyekiti wa Bodi ya Hospitali ya Ndanda, Padri Amani Nyoni anasema: "Kimaadili si sahihi kumdai rushwa ya ngono mtu aliye chini ya malezi au uongozi wako maana huyo si mkeo; huo ni uzinzi unaowaweka wote katika hatari ya kiafya kwa magonjwa mbalimbai yakiwamo ya zinaa."

Rushwa ya ngono ina madhara kiafya na kisaikolijia. Mkurugenzi wa Miracle Corners of Tanzania (MCT), Dk Katanta Simwanza anasema madhara ya kisaikolojia ni pamoja na kuondoa ufanisi katika utendaji na kusababisha msongo wa mawazo unaoweza kuleta athari ya afya ya akili na hata kusababisha vidonda vya tumbo.

"Rushwa ya ngono inaweza pia kusababisha kukosekana kwa ubinifu katika kazi; ufanisi unapungua siku hadi siku na hiyo, inaweza kuzalisha pia utoro kazini," anaongeza Dk Katanta.

Kukabili Tatizo
Vyanzo mbalimbali vinasema moja ya njia kuu za kukabili rushwa ya ngono ni pamoja na wandishi wa kike kujiamini kitalaamu na kiutendaji na kutokubali vitisho wala ahadi za upendeleo.

Mhariri wa Habari wa Gazeti la Mwananchi, Lilian Timbuka anasema ili kushinda vita dhidi ya rushwa ya ngono katika vyumba vya habari, unahitajika utamaduni imara wa uwazi wa watendewa.

"Kila chombo cha habari kiwe na sera mahsusi kuhusu masuala ya jinsia; iliyowazi na inayoeleweka kwa wote ikitamka wazi katazo la vitendo hivyo," anasema Lilian.

Mhadhiri Msaidizi katika Chuo Kikuu cha Tumaini cha Dar es Salaam (TURDAco), Kizito Noya anasema wanafunzi wanaokumbana na adha ya kudaiwa rushwa ya ngono, watumie madawati ya jinsia katika vyuo vyao kupata haki zao; wawe huru na wasikubali kurubuniwa wala kutishiwa.

"Rushwa ya ngono ama iwe chuoni, kazini au sehemu ya kutolea huduma ni tatizo juu ya tatizo katika jamii… Wandidhi wa habari wakatae rushwa ya ngono kwa kujiamini na kufanya kazi kwa viwango vya juu," anasema Kizito.

Rushwa ya ngono kwa wanahabari wanawake iko maeneo matatu

Na Sterius Sane

"Waandishi wa habari wanawake nchini wanakumbana na rushwa ya ngono wakiwa vyuoni wakisomea taaluma hiyo, wanapokuwa kwenye vyombo vya habari kufanya kazi kwa vitendo, kujitolea au wameajiriwaa na wanapokwenda kuwahoji watu ambao ni nyanzo vya habari" anesema Neville Meena, Mhariri mwanaume mzoefu na ambaye amefanya kazi kwenye vyombo vya habari kwa zaidi ya miaka 20.

Neville Meena ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) alitoa maelezo haya alipotakiwa na mwandishi huyu wa Sauti ya Siti kutoa maoni yake kuhusu ukubwa wa tatizo la rushwa ya ngono katika tasnia ya habari nchini.

"Rushwa ya ngono katika newsrooms (vyumba vya habari) ipo kwa kiasi chake, lakini tatizo hili ni kubwa mno kwa 'source' (watoa habari), kule hali ni mbaya mmno kuliko newsroom" anasema Meena.

Kauli ya Meena inaungwa mkono na anachosema Furaha Mateso (jina sio halisi?) mwandishi wa habari mwanamke aliyehitimu masomo ya Shahada ya Kwanza ya uandishi wa habari mwaka 2022 katika chuo kikuu cha Mtakatifu Augustine Tanzania (SAUT) Mwanza.

"Kwa mwandishi wa habari wa kike, rushwa ya ngono ni kama wagombea watatu katika jimbo moja maana inaanza chuoni kwa baadhi ya lecturers, inaenda newsrooms na inamfuata mwandishi wa kike hadi kwa-news sources wengine; (baadhi)', anasema Furaha na kuongeza;

"Nilianzakuhisi machungu ya rushwa ya ngono wakati ninasoma Diploma katika chuo cha (anataja chuo cha kati kilichopo Dar es Dalaam) ambapo mwalimu anaona hiki ni kipindi cha mitihani. kesho ni mtihani wa somo lake, anakuambia leo akutoe 'out".

Furaha anasema uzoefu wake wa muda mfupi katika kazi ya uandishi wa habari amegundua pia kwamba wapo baadhi ya sources, (watoa habari) ambao "wanataka wakupe stori kwa malipo ya ngono; usipokuwa makini na imara, utakuwa shemeji wa kila ofisi. kwa kweli huu ni udhalilishaji uliokuwa unanikera sana na ndio maana nilikuwa sipati hata safari za mara kwa mara kama walivyokuwa baadhi yetu na hii imenisaidia."

Kwenye vyumba vya habari, waandishi wa habari wanawake wanakumbana na rushwa ya ngono wanapokwenda kufanya kazi kwa vitendo wakiwa bado vyuoni, wanapoamua kwenda kujitolea wakisubiri kupata ajira baada ya kumaliza vyuo au wanapokuwa wameajiriwa. Uk 9

Vyombo vya habari na ushiriki katika kampeni ya kupinga Rushwa ya ngono ndani ya vyombo vya habari (Picha na TAMWA)

Uk 8

Rushwa ya ngono kwa wanahabari wanawake iko maeneo matatu

Jesca James (jina sio halisi) aliyewahi kupitia madhila hayo katika gazeti moja anasimulia alivyopokelewa alipokwenda kufanya mazoezi kwa vitendo wakati akisoma chuo kikuu.

Anasema "tulikwenda kufanya 'field' tukiwa wawili. mhariri wa habari; mwanaume (anakataa kumtaja) akawa anatuita mmojammoja. Mwanzoni nilidhani anataka kukosoa na kunielekeza namna ya kuboresha kazi zangu."

Ananukuu maneno aliyokuwa akitumia mhariri huyo kumwita akiwa na ajenda yake akisema: "Hivi huko vyuoni mnafundishwa nini! Unawezaje kuanza hivyo stori; wewe ukiwa mhariri hii stori utaielewa? Hebu njoo uisome hapa labda mimi ndiye sielewi maana mkiandikiwa ripoti mbaya mnasema mmeonewa. Nikaenda kutazama kwenye kompyuta yake ikiwa ni siku yangu ya sita ya field."

Jeska anasema tofauti maneno aliyokuta kwenye kompyuta yalikuwa: "Kwani jana hukunielewa! Si nilikwambia unisubiri jioni! Sasa leo ukitoka nitakuawa ninasubiri pale kituoni; mwache mwenzako aende nyumbani. Jitahidi usiniangushe na wewe utaanguka."

"Kutokana na ugeni tuliokuwa nao, niliona mtu wa kwanza kufunguka kwake ni mhariri msaidizi ambaye alikuwa mwanamke, Inoti Manyama (si jina halisi). Nikamwelezeza kila kitu.

Namshukuru Dada Inoti kwani siku iliyofuata, bila kutaja jina la mtu, akasema katika 'postmorterm' akisisitiza kuwa si sahihi kutumia 'ubabe' kutongoza na mambo hayo yakiendelea, atayafikisha ngazi ya juu."

Jesca anasema "huo ukawa mwisho wa vitisho hivyo, na mhariri hakutaka tena kunisemesha kwa lolote hata kunituma kazi hadi namaliza field."

Utafiti uliofanywa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) unaonyesha asilimia 48 ya waandishi wa habari wasio na ajira rasmi (correspondents) walisema wamewahi kukumbwa na visa vinavyohusu madai ya rushwa ya ngono katika vyombo vya habari.

Namna ya Kutokomeza Rushwa ya Ngono

Mwandishi Mwandamizi na Mwenyekiti wa zamani Klabu ya Wandishi wa Habari Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC), Irene Mark anasema suala la rushwa lifundishwe kuanzia ngazi ya familia ili watoto wanapokua, wajue kutoa au kupokea upendeleo kwa gharama yoyote ni rushwa na kosa linalohusu maadili.

Kwa upande wake Meena anasema dawa pekee ni wahariri kutenda kazi zao kwa wanawake waandishi wa habari kufanya kazi zao kwa bidii na kujiamini kitaaluma bila kutegemea kufanyiwa upendeleo. Amesema kwa kuzingatia hayo wanahabari wanawake watapata heshima kubwa na watatoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya taifa.

Meena amesema waandishi wa habari wanawake wana uwezo mkubwa kitaaluma ambapo baadhi wanaweza hata kuanzisha na kumiliki vyombo vya habari. Ametoa mfano wa Veronica Mrema (mmiliki wa maishanamatukio.blogspot.com) ambaye kupitia juhudi na ubora wake katika kazi, ameshinda na kunyakua tuzo mbalimbali.

Katika mahojiano Veronica Mrema anasema "nilikuwa ninafanya kazi katika chombo kimoja kama *correspondent,* lakini kulitokea tatizo lililolazimisha kutoka (hakitaji). Mmoja wa watendaji ambaye kiumri ni mtu mzima pia, akaniuliza kama kuna mtu amenitaka kimapenzi nikamkatalia."

Anaongeza "nilikuwa mkweli kwamba hakuna mtu wa namna hiyo lakini, kitendo cha kuniuliza hivyo kinaonesha moja kwa moja hilo tatizo lipo kwenye vyombo vya habari…"

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) Dk Rose anasema ili kupambana na rushwa ya ngono ni muhimu kuwepo madawati ya kijinsia katika kila chombo cha habari.

Muhimu zaidi wanahabari wote wanawake ana wanaume watambue rushwa ya ngono ni kosa la jinai.

Kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 mtu anayebainika kutumia mamlaka ya utekelezaji majukumu yake kuomba au kutoa upendeleo wa kingono, kama kigezo cha kutoa ajira, kupandisha cheo, kutoa haki au huduma, atashitakiwa chini ya Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi.

Sheria hiyo inasema mtu akitiwa hatiani kwa kosa la rushwa ya ngono, anaweza kuhukumiwa faini isiyozidi Sh milioni tano, au kifungo cha miaka 20 jela, au adhabu zote kwa pamoja.

Hata hivyo dawati la jinsia kuwepo katika kila chombo cha habari litasaidia kuzuia rushwa ya ngono endapo wanahabari wapya wote wanaume na wanawake wanapojiunga kwenye chombo cha habari wataelezwa jinsi deski hilo linavyofanya kazi, sheria inavyosema kuhusu kosa hilo na pia kama wanawake wanahabari wataelimishwa jinsi ya kukusanya ushahidi dhidi ya kosa la rushwa ya ngono.

Rushwa ya ngono:
Fikiria hatma ya uandishi wa habari Afrika bila wanawake

Na Dkt. Rose Reuben

Rushwa ya ngono ni kitendo kiovu kinachosababisha waandishi wa habari wanawake wengi Barani Afrikakukimbia taaluma yao na hivyo kuhatarisha hatma yao na maendeleo ya nchi zao

Mercy Njoroge kutoka shirika la wanahabari wanaotetea haki za binadamu Kenya amesema takwimu za Chama Cha Wachapishaji wa Habari Ulimwenguni (WIN-IFRA) zinaonyesha asilimia 41 ya wanahabari wanawake wamefanyiwa vitendo vya unyanyasaji wa kingono kwa maneno au kimwili wakiwa katika sehemu zao za kazi. Kutokana na ukubwa wa tatizo hili, hivi sasa kuna juhudi za kimataifa zinaendelea kwa lengo la kuhakikisha rushwa ya ngono inakomeshwa barani Afrika.

Kwa mfano, Amina Mohamed kutoka shirika la misaada la Canada linalojulikana kama Camera for Girls amesema shirika hilo limekuwa likishirikiana na vyuo vikuu Barani Afrika kuwajengea uwezo wanawake wapate kazi bila kulazimika kutoa rushwa ya ngono katika kazi ambazo zimekuwa zikishilikiwa zaidi na wanaume.

Amina amesema amewasikia baadhi ya wanafunzi wanahabari wanawake katika baadhi ya nchi za Afrika wakilalamika kuwa wanakumbana na unyanyasaji wa kingono wanapokwenda kufanya mafunzo kwa vitendo kwenye vyombo vya habari.

Anasema “ni ujinga kwa mtu mwenye ujuzi kuombwa kutoa fedha au kutoa rushwa ya ngono ili kupata kazi… ndiyo maana tunafundisha pia wanafunzi jinsi ya kusema HAPANA kwa unyanyasaji wa kimfumo.

Kudhibiti rushwa ya ngono kwenye vyombo vya habari ni muhimu kwa sababu ikiachwa iendele inaweza kupelekea wanahabari wengi wanawake kutojiunga na taaluma hii na walioingia kuondoka.

» Uk 11

Kulia ni mmoja wa wanahabari wanawake akiwa katika moja ya majukumu yake.

Uk 10



Fikiria hatma ya uandishi wa habari Afrika bila wanawake...

“Ninaweza kufikiria chumba cha bahari bila waandishi wa habari wanawake, watu wenye ujuzi na utashi wa kuandika habari kwa mtazamo wa usawa wa jinsia watakuwa wameondoka kwenye vyombo vya habari”,anasema Wenceslaus Mushi ambaye amefanya kazi kwenye vyombo vya habari kwa miaka 45.

Mushi anasema anafahamu madhara ya vyombo vya habari kutokuwa na waandishi wa habari wanawake kwa sababu aliwahi kufanya kazi katika chumba cha habari ambacho kilikuwa na waandishi wa habari wanawake wawili tu lakini baadaye mmoja akaondoka kwenda masomoni na mwingineakapata kazi nyingine yenye malipo makubwa.

“Kwa miaka saba kabla ya kuajiri tena wanawake chomba chetu cha habari kilikuwa kinachapisha habari ambazo zilikuwa hazionyeshi hali halisi ya wanawake na wanaume kwa sababu habari zilizokuwa zinahusu masuala ya wanawake zilikuwa hazipewi umuhimu”, anasema Mushi.

Maoni ya Mushi yanaungwa mkono na Abdallah Majura ambaye aliwahi kuwa mmiliki wa chombo cha habari na mwandishi ambaye amefanya kazi kwenye vyombo vya habari kwa zaidi ya miaka 34.

Majura anasema ‘sekta ya vyombo vya habari bila wanawake, daima itakuwa mazingira ya kuchosha kufanya kazi na taaluma itakwama”.

Majura anasema vyombo vya habari lazima viwe na waandishi wa habari wanawake na wanaume ili viweze kuandika habari kwa ufanisi kuhusu masuala mbali mbali yakiwemo yale yanayoathiri wanawake kwa mfano vifo vya uzazi na ukeketaji.

Hata, hivyo, endepo rushwa ya ngono haitatokomezwa kuna uwezekano siku zijazo taaluma ya habari barani Afrika ikakosa wanawake na hivyo kukosa habari za masuala tofauti yanayohusu maendeleo ya wanawake.

Ripoti za utafiti kutoka vyuo vikuu vya uandishi wa habari na mawasiliano zinaonyesha kwamba wasichana wengi wanajiunga na vyuo hivyo na kuhitimu kila mwakalakini ni wachache tu wanabaki kufanya kazi katika vyombo vya habari.

Wengine wanaamua kufanya kazi za mawasiliano ya umma ambapo pia wanakuwa hawana furaha, wengine wanahamia katika fani nyingine ikiwepo ujasiriamali na wengine huishia kuwamama wa nyumbani. Uk 12

Fikiria hatma ya uandishi wa habari Afrika bila wanawake

Patricia Ibasi kutoka Mtandao wa Wanahabari wanawake Sudani ya Kusini anasema unyanyasaji kijinsia na wa kingono unaendelea barani Afrika kwa sababu kitamaduni wanawake hawafichui maovu wanayofanyiwa.

Mambo maovu wanayofanyiwa wanawake ni pamoja na kupigwa na kuingiliwa kingono kwa sababu jamii inachukulia maovu dhidi ya wanawake kuwa ni mambo ya kawaida lakini yanayoweza kusababisha ulipizaji kisasi kwa wahalifu.

Kuhusu kipengele cha kitamaduni kinachochochea rushwa ya ngono Majura anasema changamoto ni dhana kuwa wanawake wanaofanya kazi kwenye vyombo vya habari ni wanawake tu ambaowanahabari wanaume wanaweza kuwafanyia jambo lolote wanalotaka.

“Lakini hii ni makosa kwa sababu vyumba vya habari ni sehemu ya kazi ambapo watu wanapaswa kuwasiliana kitaaluma na siyo vinginevyo”, anasisitiza Majura.

Shirika la African Women in Media na Fojo, International Women’s Media Foundation, Women News na utafiti uliofanywa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA)kati ya mwaka 2019 hadi 2021 ulibaini ukosefu wa kutokuungwa mkono kwa wanawake kushika nafasi za maamuzi katika vyombo vya habari.

Hii inaweza kuwa sababu mojawapo wanawake wanahabari wanapoombwa rushwa ya ngono wanakuwa hawaripoti kwenye vyombo vya sheria ili sheria ichukue mkondo wake badala yake huamua kukaa kimya.

Ibasi anasema wanawake huko Sudan ya Kusini wakipatwa na madhila ya kuombwa rushwa ya ngono huwa wanakaa kimya badala ya kuriripoti jambo hilo ili hatua sahihi zichukuliwe.

Amesema “inawezekana wananyamaza kimywa kwa sababu wanaogopa mambo kadha wa kadha, labda wanalinda ajira zao, unajua kuna mashirika mwengi ya habari Sudani Kusini ambayo yanakuwa yanazungunza rushwa ya ngono kichinichini tu”, na anaongeza,

“Lakini waandishi wa habari wanawake hawazungumzii tatizo hili kwa uwazi na hawataki kujitokeza kulizungumzia kwa sababu wanadhani ni utamadun… si unajua..”

Ndiyo sababu katika miaka ya 1980 waandishi wa habari wanawake wachache nchini Tanzania waliamua kuanzisha TAMWA ili kuvikabili vikwazo hivi ana kwa ana na kuandika upya simulizi za historia ya mapambano ya wanawake.

Madhumuni ya kuwajengea uwezo wanawake katika vyombo vya habari ni kuhakikisha wanafikia uwezo wao kamili wa juu mahala pa kazi na kuongezeka kwa kiasi kikumbwa sauti za wanawake katika maudhui ya vyombo vya habari.

Kiukweli, Afrika lazima tuhakikishe taaluma ya uandishi wa habari inajumuisha wanawake na wanaume. Waandishi wa habari wanawake ni muhimu kwa sababu haki za binadamu ni haki muhimu.

Kwa kweli. Afrika lazima tuhakikishe taaluma ya uandishi wa habari inajumuisha wanawake na wanaume Waandishi wa habari wanawake ni muhimu kwa sababu haki za binafamu ni hakimuhimu.

Hii ndiyo sababu mwaka 1980 wandishi wachache nchini Tanzania waliamua kuanzisha TAMWA kwa lengo kwa lengo la kuhoji na kuviondoa hivi vikwazo kuandika historia mpya.

Kwa kweli katika bara la Afrika ni muhimu tuhakikishe taaluma ya uandishi wa habari inajumuisha wanawake na wanaume. Hii ni kwa sababu waandishi wa habari ni muhimu kwa vile haki za binadamu za wanawake ni muhimu.

Wanahabari wanawake watakuwa ni watu muhimu kila wakati kwenye vyombo vya habari kwa sababu wanaleta mitazamo tofauti kwenye habari na wanahakikisha uwakilishi wa sauti za wanawake kwenye habari.

Vile vile wanaripoti habari kwa usawa wa kijinsia, wanakuwaniwanawakewamfanowakuigwa,wanapinga dhana potofu dhidi ya wanawake,wanashirikiana na watazamaji na wanachangia uandishi wa habari shirikishi na unaovutia.

Kwa hiyo, nchi zote za Afrika, zinahitaji kutokomeza rushwa ya ngono katika vyombo vya habari kwa sababu mchango wa waandishi wa habari wanawake unatoa taswira nzuri kwa vyombo vya habari na kusaidia kutatua changamoto na wasiwasi walionawao wanawakewaandishi wa habari.

Rushwa ya ngono inavyochochea wanahabari wanawake kuwa tegemezi kiuchumi

Na Shadida Dalanga

"Rushwa ya ngono ni rushwa hatari sana kwa wanawake wakiwemo waandishi wa habari maana kila mahali na kila wakati inawasukuma katika shimo la utegemezi kiuchumi."

Anasema Mtaalamu wa Masuala ya Jinsia, Afya, Uzazi, Familia na Malezi, Dkt Katanta Simwanza wakati akizungumza na SAUTI YA SITI kuhusu janga la rushwa ya ngono dhidi ya waandishi wa habari wa kike katika vyumba vya habari nchini.

"Wanawake wengi wakiwemo waandishi wa habari wanaogopa kuomba kazi kwenye taasisi mbalimbali kwa kuwa wanakumbana na 'kisiki' cha kudaiwa rushwa ya ngono."anasema Simwanza na kuongeza;

"Wengine wakiwemo ambao hawajaajiriwa na walio katika mafunzo kwa vitendo wanadaiwa rushwa hiyo huku wakipewa ahadi bandia kuwa wakikubali, watapata ajira haraka na kirahisi na pia, watapata mshahara mnono na wataishi kwa raha katika mazingira ya kazi."

Maneno ya Dkt Katanta yanafanana na ya Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA-TAN), Salome Kitomari anayesema rushwa ya ngono inachochea utegemezi wa kiuchumi kwa waandishi wa habari wanawake.

Kitomari anasema kwa mfano "shirika fulani linaweza kuandaa safari kwa waandishi kwenda kuandika habari zenye maslahi kwa taifa, lakini baadhi ya watu katika shirika hilo, wakatumia hiyo nafasi kutaka 'kuwapata' waandishi kiurahisi ili wawatumie kingono".

Kadhalika anasema "mwandishi akishafanyiwa hivyo mara moja wakati mwingine ikitokea safari anaogopa kwenda akihisi hali itakuwa ile ile na hivyo".

Kwa sababu hiyo, "mwandishi huyo anakosa fursa ya kupata fedha za kuboresha uchumi wake ambazo anngelipwa kwa kushiriki katika kuripoti stori kwenye hilo shirika", anasema Kitomari..

» Uk 14

Uk 13

Rushwa ya ngono inavyochochea ...

Salome anatoa mwito kwa waandishi wa habari wanawake kupambana na hali ya adha hiyo wanapokutana nayo kwani wanapofanikiwa kuvuka viunzi hivyo, huwa imara zaidi na hufanya kazi bila kuyumbishwa.

Mtaalamu wa Masuala ya Uchumi na Habari, Rosemary Mwakitwange anasema mzizi wa rushwa ya ngono kwenye vyombo vya habari unaanzia vyuoni wanapoandaliwa kabla ya kuingia kwenye tasnia.

"Vyuo vingi nchini havina mifumo ya ufundishaji inayomuwezesha mwanahabari kujiamini baada ya kumaliza masomo vyuoni", anasema Mwakitwange na kuongeza;

"Hali hii inayowafanya baadhi wafikapo kwenye vyumba vva habari, wahitaji upendeleo ili kupata nafasi,"

"Baadhi ya wandishi wa habari wanawake wala hawaelewi kwamba ni hasara kwao kama mtu mwingine ataandika habari kisha akamuwekea jina lake ili aonekane kuwa ndiye kaandika kwa kubadilishana na rushwa ya ngono. Hali hii inasababisha utegemezi kitaaluma, kiutendaji na kiuchumi," anasema.

Mifano hii ya rushwa ya ngono kuwafanya wanahabari wanawake kuwa tegemezi inamgusa mmoja wa waandishi wa habari wa kike katika gazeti moja la kila siku Nyanyumbu Matiga (Si jina halisi) anayeshuhudia yaliyomfika.

"Kila alipokuwa akiniita ofisini kwake; kubwa aliloanza kuhoji ni kusema, 'hivi nyongeza ya mshahara ya mara nne unaiona ni kitu kidogo na kwamba si bahati ya kipekee iliyo mbele yako?, anasema Nyanyumbu.

Anasema kiongozi wake ambaye si mwandishi wa habari bali ni meneja wa rasilimali watu, kila alipokuwa akimwita ofisini kwake, alikuwa akimhimiza kuwa, endapo atakubali kushiriki naye mapenzi, atamwongezea mshahara mara nne ya ule aliokuwa akipokea.

Anasema "huyo meneja mwajiri; alikuwa ananiambia nipo vizuri; nitenge muda wa kukaa naye baada ya kazi ili anielekeze jinsi ya kuwa mwandishi bora ingawa yeye taaluma yake si habari."

"Kilichonishangaza ni kuwa, nilipokuwa nikikutana naye alikuwa haongelei mambo ya kazi, bali kunisifia na kuniahidi hata kunipandisha cheo haraka eti kwa kuwa mimi ni mrembo", anaongeza.

Nyanyumbu anasimulia kuwa, siku moja bosi huyo alimwambia amsubiri ili amwelekeze cha kufanya siku inayofuata. Anasema alitekeleza aliloambiwa hivyo, jioni akapokea simu ikimtaka aende ofisini kwa bosi huyo.

"Nilipoingia ofisini kwake, akaanza tena kunishikashika, lakini safari hii 'akaanza kuzidisha mazoea' maana sasa alinishika kiuno na kutaka kunishika matiti," anasema na kuongeza: "… siku hiyo nikashangaa anafunga mlango na kuanza kuvuta sketi yangu kuishusha chini," anasema.

Anaongeza "ilibidi nimlaghai kwa kumwambia avae kinga maana sina muda wa kubeba mimba sasa hivi. Akaamini na alipoinama kwenye droo ya meza yake labda kuangalia kama kuna kondomu, nikafungua haraka mlango na kutoka."

Nyanyumbu anasema kadhia hiyo ilimsababishia sonona na hatimayeakaamua kuachana na taaluma ya habari aliyoisomea na badala yake akaanza kujishughulisha na biashara ndogondogo.

Anasema "huyo meneja mwajiri; alikuwa ananiambia nipo vizuri; nitenge muda wa kukaa naye baada ya kazi ili anielekeze jinsi ya kuwa mwandishi bora ingawa yeye taaluma yake si habari."

KOSA ANALOJUTIA

Nyanyumbu anasema anajuta kwa kukosa ujasiri wa kukataa moja kwa moja na kwa ukali tangu siku ya kwanza na kwamba, kosa la kuruhusu mazoea akidhani 'anamzungusha tu' ndilo lilikuwa linamponza.

"Ninajuta maana nilipaswa nikatae mapema na nitoe taarifa kwenye mamlaka husika" alisema Nyanyumbu.

RUSHWA YA NGONO INAVYOTAZAMWA

Kwa mujibu wa Kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007 (PCCB Act, 2007), rushwa ya ngono hujitokeza pale mtu aliye katika mamlaka na katika kutekeleza mamlaka yake, anataka au anaweka upendeleo wa ngono kama kigezo cha kutoa ajira, cheo, haki, au huduma ya upendeleo.

Uk 15

Uk 14

Rushwa ya ngono inavyochochea ...

Kimsingi, rushwa ya ngono imekuwa ikiathiri watu wengi hasa wanawake wakiwamo wanahabari kwa hadi kushusha ufanisi katika utendaji kazi wao.

Chapisho la taasisi ya Door of Hope Tanzania liitwalo 'Ijue Rushwa ya Ngono' lililopo mtandaoni limeandika: "Tofauti na vitendo vingine vya ukatili wa kingono, rushwa ya ngono inashinikizwa bila kutumia nguvu moja kwa moja."

Linasema "wakati mwingine, rushwa ya ngono haihusu vitendo vya kujamiiana tu, bali pia mambo mengine ya unyanyasaji wa kingono kama kulazimishwa kupigwa picha za ngono na kupapaswa mwili na hutokea penye uhusiano wa kimamlaka kati ya mdai na mwathirika wa rushwa ya ngono."

Kwa mujibu wa tathmini ya awali iliyofanywa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) chini ya mradi wa kutoa elimu na mafunzo kuhusu rushwa ya ngono katika vyombo vya habari uliofadhiliwa na WFT-T na kufanyika Dar es Salaam, asilimia 48 ya waandishi wa habari wasio na ajira rasmi walisema wamewahi kukumbwa na visa vinavyohusu madai ya rushwa ya ngono katika vyombo vya habari.

Kutokana na tathmini hiyo, asilimia 52 hawakuwa tayari kusema lolote kuhusu rushwa hii.

Ilibainisha kuwa, waathirika wakubwa wa rushwa ya ngono katika vyumba vya habari ni waandishi wahabari wanawake wanaolipwa kwa idadi ya ripoti au makala wanazoandika, wanaojitolea kabla ya kuajiriwa na wanafunzi walio katika mafunzo kwa vitendo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA Dkt Rose Reuben alisema ipo haja ya kuwa na sera itakayodhibiti rushwa ya ngono katika vyumba vya habari ikiambatana na ukumbusho wa mara kwa mara juu ya suala hilo.

"Tatizo kubwa katika vita dhidi ya rushwa ya ngono, ni ukimya unaotokana na waathirika kuhofia kuwa, watenda kosa watasikilizwa zaidi kuliko waathirika ambao wataambulia unyanyapaa," anasema .

ATHARI

Vyanzo mbalimbali vinasema rushwa ya ngono dhidi ya wanawake wakiwamo wandishi wa habari ni pamoja na kugeuza haki kuwa upendeleo hali inayosababisha baadhi ya wasio na uwezo kuajiriwa huku wenye sifa wakiachwa.

Athari nyingine ni kumnyima mlengwa (mwathirika) haki za kikatiba, kudhalilisha utu na afya ya mwanamke, kudumaza taaluma na uchumi na kuathiri vibaya harakati za ukombozi wa mwanamke.

YAPASWAYO KUFANYIKA

Dkt. Katanta anasema serikali na wadau mbalimbali wanapaswa kutoa elimu kuhusu sheria ya kudhibiti rushwa ya na kuhakikisha wanaopatikjana na hatia wanaotenda kosa hilo wanaadhibiwa kikamilifu.

"Zianzishwe njia salama zenye usiri na zinazofikika kirahisi kwa kila mtu kuripoti masuala ya rushwa ya ngono ili waathirika wa vitendo hivyo watoe taarifa bila vikwazo," anasema Katanta.

Naibu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) katika Mkoa wa Kinondoni jijini Dar es Salaam Elizabeth Deborah Mokiwa anakiri jitihada zao kukwamishwa na usiri uliogubika uhalifu wa rushwa ya ngono.

Anasema inashangaza kuona wanahabari hawaripoti vitendo vya madai ya rushwa ya ngono wanapokumbana navyo.

"Uanahabari wako unatosha kukupatia cheo au mshahara mzuri; usikubali mwili wako utumike kuongeza sifa ya kupata unachostahili, acha utendaji wako wa kazi ukupandishe na si vinginevyo," anasema Elizabeth.

Anaahidi TAKUKURU mkoani Kinondoni ni kuanzisha programu maalumu ya kuelimisha wanahabari madhara na namna ya kukusanya ushahidi na kuripoti matukio ya rushwa ya ngono.

Rushwa ya ngono kwenye vyombo vya habari:

Safari bado ndefu

Na. Zahara Tunda, Dodoma

Suala la rushwa ya ngono katika maeneo ya kazi si kitu kipya ulimwenguni, na wanawake wamekuwa ndio wahanga wakubwa kuliko wanaume.

Kwenye vyombo vya habari rushwa ya ngono ni kero inayowasumbua zaidi wanawake ambao wanachipukia katika taaluma hiyo.

Kwa ngazi za dunia, takwimu za shirika la Women in News(WIN-IFRA) zinaonyesha kwamba asilimia 47 ya wanawake katika vyombo vya habari wamekumbana na unyanyasaji wa kingono wakiwa kwenye maeneo yao ya kazi.

Kati ya wanawake waliokumbana na unyanyasaji wa kingono asilimia 56 kati yao walinyanyaswa kwa kutumia maneno wakati asilimia 38 walifanyiwa vitendo vya kingono katika maeneo yao ya kazi.

Hapa Tanzania, utafiti uliofanywa na Chama cha Waandishi wa habari Wanawake Tanzania (TAMWA) mwaka 2021 unaonyesha asilimia 48 ya waandishi wa habari wasio na ajira rasmi maarufu 'correspondent' wamewahi kukumbwa na visa vinavyohusu madai ya rushwa ya ngono katika vyombo vya habari.

Mwandishi wa makala hii ya Sauti ya Siti amezungumza na mwandishi wa habari Doris Damian 30 (Sio jina lake kamili)aliyepitia changamoto ya unyanyasaji wakijinsia katika chombo cha habari, mkoani Dodoma nakuona chungu tamu ya

Mmoja wa wahanga wa rushwa ya ngono ndani ya vyombo vya habari (jina limehifadhiwa) (PICHA NA TAMWA)

Sauti ya Siti: Hili suala lilianzaje?

Doris: Suala hili lilianza pale nilipofika katika kituo changu cha pili cha kazi tangu nilipoanza taaluma hii. Katika dawati la habari mhariri wangu alikuwa ni mwanaume hivyo nilikutana na changamoto zilizoashiria ni unyanyasaji wa kingono ikiwemo kuzuiwa kutoka kazini kwa muda uliopangwa ambapo unaweza kupata usafiri wa ofisi.

» Uk 17

Uk 16

Rushwa ya ngono kwenye vyombo vya habari: Safari bado ndefu ...

Sauti ya Siti: Hali hii iliendelea kwa muda gani?

Doris: Ilichukua muda mrefu kidogo mpaka nilitamani kuacha kazi kituo kile ili nikatafute mahali pengine kwaajili ya usumbufu huo. Lakini nilipomshirikisha baba yangu wa kiroho aliniambia nisiondoke ila niendelee kumuomba Mungu adhihirishe hatma yangu kwamba natakiwa kuwa wapi.

Sauti ya Siti: Wewe kama mwandishi wa habari ulikuwa unajisikiaje kwa kipindi hiko?

Doris: Nilijisikia vibaya sana hapa ndo pale lile neno la 'Why me' linapofanya kazi.Hata hivyo,nilizidi kuomba Mungu na kujipa moyo kwamba hata mimi naweza kuvuka katika hili.

Sauti ya Siti: Je aliwahi kukushika maungo au kukulazimisha kufanya chochote bila idhini yako?

Doris: Kunishika mabega nakulazimisha kunikumbatia.

Sauti ya Siti: Je ulichukua hatua gani kufuatia tukio hilo?

Doris: Kwa kweli niliongea na baadhi ya watu hapo ofisini wakasema ndo tabia za hapo kituoni. Kwahiyo niliendelea kuomba tu Mungu anisaidie kuniepusha na hilo kwa sababu sikuwahi kuwaza kuutumia mwili wangu kwaajili ya kupata kitu chochote na nilipoenda pale nilikuwa ninajitolea tu sikuwa mwajiriwa. Lakini Mungu akafanya na mimi nikaajiriwa, aliona aibu sana maana alisema bila yeye siwezi kupata ajira kwasababu yeye ndiye anaweza kuongea na boss na si mtu mwingine.

Sauti ya Siti: Je ulipata changamoto zozote za kiakili ulipopitia unyanyasaji huo?

Doris: Changamoto zipo kama hizo za kuanza kuwaza labda niache kazi hapo ili niepukane nao. Ile hali haikutoweka kirahisi kwani niliamini katika misimamo yangu na kwa msaada wa Mungu.

Sauti ya Siti:Je ni kwanamna gani tukio hilo limeathiri utendaji wako wa kazi?

Doris: Utendaji wa kazi ulianza kusuasua hasa katika uandaaji wa habari zangu, maana adui ndio yupo katika dawati. Wakati mwingine unanyimwa tape recorder unapotaka kwenda kufanya kazi zako za vipindi nje ya ofisi.

Sauti ya Siti: Unafikiri nini kifanyike kupunguza au kutokomeza masuala ya unyanyasaji wa kingono kwenye vyombo vya habari?

Doris: Kitu kikubwa kinachotakiwa kufanyika kwasasa ni wanahabari wanawake kuimarisha uwezo wao wakufanya kazi kwa weledi na kujiamini katika utendaji wao wa kazi.. Muhimu kila Mmoja amtegemee Mungu kwakiasi kikubwa sana, kwani kuna majaribu mengine katika mahali pa kazini magumu hasa kwa sisi ambao hatukuwahi kuwaza na kuwa na mahusiano mahala pa kazi.

Kupitia kisa cha Doris tunaona jinsi suala la rushwa ya ngono linaweza kukatisha mtu tamaa ya kufanya kazi kama akikosa watu sahihi wa kuwakimbilia na kupata ushauri sahihi.

Hata hivyo, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) hawako nyuma katika kuhakikisha wanawasaidia waathirika kwakuwapa ushauri nasaha kuwaponya kisaikolojia, nakuwaelekeza maeneo ambayo wanaweza kusaidiwa kama vile TAKUKURU.

"Endapo mtu atahitaji kuripoti unyanyasaji wa kingono anakuja na kusema tatizo lake na pia anaweza kutuma tamwa@tamwa.org japo mpaka sasa hatuna hotline ambayo mtu anaweza kutuma ujumbe wake moja kwa moja." Amesema Dkt. Rose Reuben Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA.

Rushwa ya ngono ni kosa la jinai. Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 katika Kifungu cha 25 inasema, mtu anayebainika kutumia mamlaka ya utekelezaji majukumu yake kuomba au kutoa upendeleo wa kingono, kama kigezo cha kutoa ajira, kupandisha cheo, kutoa haki au huduma, atashitakiwa chini ya Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi.

Mtu akitiwa hatiani kwakosa la rushwa ya ngono, anaweza kuhukumiwa faini isiyozidi Sh milioni 5, au kifungo cha miaka 20 jela, au adhabu zote kwa pamoja.

‘Rushwa ya ngono inatutesa wanahabari tunaojitolea’

Na Sauda Msangi

“Waandishi wa habari wanawake tunaofanya kazi kwa kujitolea tukisubiri nafasi za ajira tunapitia mateso mengi kwasababu tunapitia mitego mingi ya rushwa ya ngono”, anasema mwanahabari mwanamke Nangasu Majidy (si jina halisi) mwenye umri wa miaka 28.

Waandishi wa habari wakiwa katika mahojiano na chanzo cha habari

Mwandishi huyu ambaye ni mhitimu wa Shahada ya Kwanza ya Mawasiliano ya Umma katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine cha Tanzania (SAUT) Mwanza alisema haya alipoombwa na mwandishi wa makala kuzungumzia anavyofahamu kuhusu adha ya rushwa ya ngono katika vyumba vya habari nchini.

Anasema “kwa mfano, mimi najiona kama mwenye mkosi na niliyepoteza muda wangu kwenda chuo cha uandishi wa habari maana badala ya kuvuna matunda, naona ninaambulia machungu kana kwamba kuwa mwanamke ndilo kosa langu. Hata hivyo, katu sitakata tamaa.”

Anaeleza “adha kubwa kuliko zote, ni ubaguzi, udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia; hasa kero ya kulazimishwa kufanya ngono na bosi ili upate haki hata unazostahili kadiri ya vigezo na uwezo wako kiutendaji”.

Anaongeza “ndiyo maana waandishi wanawake wakifika tu chumba cha habari, inawezekana wakapokelewa kwa ukali na vitisho, au kwa ukarimu ambao kila unapo utathmini, unaona kabisa siungwana, bali kuna jambo linalotafutwa tena kwasharti la mapenzi.”

» Uk 19

Uk 18

‘Rushwa ya ngono inatutesa wanahabari tunaojitolea’

Nangasu anasema licha ya kujiamini mwenyewe huku watu wa kisifia kazi zake, ameendelea kutumikishwa kama mwandishi wa kujitolea huku wenzake wakiwamo waliomkuta, wakipata ajira rasmi.

Anasema “vyeti vyangu ni vizuri kabisa, uwezo wakutafuta stori nakuiandika vizuri ninao na ndiomaana mara nyingi kazi zangu zinatoka ‘front page’ (ukurasa wa mbele), tena situ za kutumwa au kusubiri mikutano, bali hata za kujituma nakufanya uchunguzi mwenyewe…”

“Hili limekuwa likiniumiza sana maana niliyoyaacha kwenye kampuni ya kwanza, ndiyo ninayokutana nayo huku maana kote wahariri ni wanaume na nikama wanaambizana ni kama nimeruka tope na kukanyaga tope lingine,” anasema Nangasu..

Amefafanua kwamba hali hiyo inachangia umaskini na utegemezi kwa wanahabari wanawake. Amesema kwa mfano ingawa wanaojitolea hawana malipo rasmi, wanalazimika kwenda nakurudi kwenye maeneo ya kazi kwa gharama zao.

Anaongeza: “kwakweli lazima uwe imara ushinde udhalilishaji huu.“

Mhariri wa Habari wa gazeti la Mwananchi, LilianTimbuka anasema rushwa ya ngono inawafanya baadhi ya waandishi wa habari wanawake kuwa wategemezi kiuchumi kwasababu kwani licha ya kuwa na sifa stahiki, wapo hawataki kuomba kazi katika vyombo vya habari kwa kuofia kulazimishwa kutoa rushwa ya ngono.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk Rose Reuben anasema kutokana na rushwa ya ngono waandishi wa habari wanaoonekana katika vyumba vya habari ni wachache ingawa wapo wengi waliosoma taaluma hiyo.

Mmoja wa wahariri wanaume Joseph Sabinus ambaye ni Mratibu wa Gazeti la Habari LEO Afrika Mashariki, anasema mtumishi anaendekeza rushwa ya ngono akitaka rushwa ya ngono atamfokea mwandishi wa habari wanawake anayetaka ampe hiyo rushwa.

Pia amesema mtu mwenye mamlaka kwenye chumba cha habari akiomba rushwa ya ngono anaweza akaamua kutokuzichapisha habari anazoziandika aliyekataa kutoa rushwa bila sababu ya msingi.

Sabinus amesema “katika vyombo vya serikali, rushwa ya ngono siyo kubwa kutokana na mfumo wa ajira, nyongeza ya mishahara na safari huwa zinatolewa kwa kufuata mchakato rasmi unaoshirikisha watendaji mbalimbali wa kike na wakiume.”

Kwa mujibu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), rushwa ya ngono imewekwa katika makosa ya uhujumu uchumi chini ya Kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

Kifungu hicho kinasema anayebainika kutumia mamlaka yake ya utekelezaji majukumu kuomba au kutoa upendeleo wa kingono, kama kigezo cha kutoa ajira, kupandisha cheo, kutoa haki au huduma, atashitakiwa na akitiwa hatiani, anaweza kuhukumiwa kulipa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo cha miaka 20 jela, au adhabu zote kwa pamoja.

Mwaka 2020, shirika la WAN-IFRA (Women in News -WIN) liliazimia kuchambua ukubwa wa unyanyasaji wakingono katika mashirika ya habari na kupima ufanisi katika kuudhibiti.

Lilifanya utafiti katika nchi nane barani Afrika ikiwamo Tanzania. Botswana, Malawi, Kenya, Rwanda, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

Matokeo yanaonyesha kuwa, asilimia 47 waliohojiwa walikuwa wamenyanyaswa kingono kazini.

Kwa mujibu wa utafiti huo, wanawake walikuwa nauwezekano mara mbili wakupata unyanyasaji wa kijinsia kazini kuliko wanaume.

Aidha, kati ya mameneja 32 waliohojiwa, zaidi ya nusu walikuwa wamenyanyaswa kingono na kati yao, watatu pekee ndio walioripoti tatizo hili hali inayoonesha kuwa, unyanyasaji wa kijinsia ukiwamo wa madai ya rushwa ya ngono umegubikwa na ukimya.

Aidha, tathimini yaawali iliyofanywa TAMWA mwaka 2021 kuhusu rushwa ya ngono katika vyombo vya habari Dar es Salaam ilibainisha kuwa, asilimia 48 ya waandishi wa habari wasio na ajira rasmi kwenye vyombo vya habari walisema wamewahi kudaiwa watoe rushwa ya ngono.

Kwa nyakati tofauti, Dk Rose wa TAMWA na Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Neville Meena wamesema rushwa ya ngono, husababisha wanawake wengi waliosomea uandishi wahabari kuachana na taaluma hiyo na kufanya kazi nyingine.

“Rushwa ya ngono hugeuza haki kuwa upendeleo na husababisha wasio na uwezo kuajiriwa nakuachwa wenye sifa sitahiki. Hii ni mbaya sana.”anasema Dr. Reuben.

Baadhi ya wanahabari katika mikoa ya Arusha, Mwanza na Dodoma wanasema moja ya njia bora ya kukabili rushwa ya ngono katika vyumba vya habari, ni viongozi wa vyombo makao makuu kuzungumza mara kwa mara na wandishi wa mikoani, wanaume na wanawake kujua changamoto zao ikiwa ni pamoja na unyanyasaji kingono.

Mhariri Mkuu wa Redio FreAfrika (RFA) na Meneja wa Rasilimali Watu wa kampuni ya Sahara Media, Sharban Ally anasema “inabidi kila chombo cha habari kinahitaji kuwa na sera zilizowazi kwa watu wote na mifumo maalumu ya wanahabari kutolea taarifa kuhusu matukio ya rushwa ya ngono.”

“Najuta kukubali rushwa ya ngono”

Na Vicky Kimaro

“Mabosi walinishawishi kwa pesa, starehe za gharama, bia na nyama choma, niliwekwa kwenye timu ya watu wakuripoti stori kubwa, nilijiona mimi ndio mimi,lakini leo ninajuta niliingia mtego wa rushwa ya ngono”.

Hivi ndivyo anavyoanza kueleza Zawadi John (Sio jina lake halisi) kuhusu uzoefu wake kuhusu kosa la rushwa ya ngono.

Anasema “kazi zenye hela nilipewa mimi, wengine walienda mbali na kuandika habari nakuweka jina langu kama vile ni mimi nimeiandika”.

Anaongeza “kuna wakati baadhi ya wafanyakazi wenzangu wa kike walilalamika kuwa napendelewa, kwakuwa wakati mwingine ‘story’ ni yafulani lakini ‘byline’ napewa mimi, walipolalamika mimi sikujali…”.

Anasema wapo watumishi waliojikuta wakiingia matatizoni, kwa ‘kupigishwa mswaki’ yaani hawapangwi kazi, na wakileta kazi hazitoki au zikitoka lakini inaonyeshwa zimeandikwa na “Mwandishi Wetu” badala ya jina la aliyeiandika.

Zawadi anasema “hii yote ilitokana nakupinga baadhi ya vitu ambavyo waliona haviendani na maadili ya kazi, hususani kwa yaliyokuwa yanaendelea kwa upande wangu”.

Siku ambayo hataisahau

Zawadi anasema “iko siku naikumbuka vizuri sitaisahau, dada Mmoja anaitwa J, yupo kwenye tasnia ya habari mpaka sasa, ni dada mstaarabu, ni muwazi na mwenye misimamo, kuna siku aliniita ilikuwa ni Jumamosi”,

Anasema akaniambia “Zawadi wewe ni mrembo, kila mwanaume anatamani kuwa na wewe, lakini sio kwamba wanakupenda, wanakutamani tu kwasababu wengi wana wake zao”.

Anasema huyo dada J. alimwambia “watakuchezea nakukuacha, wakikukinai hii ofisi utaiona chungu”.

“Zawadi anasema dada J alimwambia “kwa kifupi wanachofanya ni kukuchezea, siku isiyo najina utakuja kujutia hiki unachokifanya, utaondolewa kwaaibu, acha hicho unachokifanya, tulia wewe ni binti mrembo, usitumie uzuri wako vibaya”. Uk 21

Wadau wa masuala ya kijinsia wakiwa katika kongamano la maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

Uk 20

“Najuta kukubali rushwa ya ngono”

Anasema alimsikiliza dada J akaachana na mabosi wawili, lakini alishindwa kuhimili presha kubwa aliyokuwa akiipata kwa bosi mkubwa ndani ya Kampuni ile, ambaye alimtishia kumfukuza kazi iwapo atakwenda kinyume na matakwa yake, huku pia akimuahidi vitu vingi ikiwemo kumpatia ajira ya kudumu.

Zawadi anasema wakati akifanya hayo alikuwa simuajiriwa bali mtu wakujitolea akilipwa kutokana na story, hivyo alipata ahadi kemkem ikiwemo kupatiwa ajira na kuishi kama malkia katika ofisi ile.

Anasema siku moja kukatokea mgogoro kati yake na bosi mkubwa baada ya kubeba ujauzito wa mwanaume mwingine.

“Kadri mimba ilivyokuwa nauhasama kati yangu na bosi mkubwa ukazidi, bahati mbaya zaidi na mwanaume aliyenipa ujauzito kwa ahadi ya kunioa, kuninunulia gari na kunijengea nyumba akatoweka”, anasema.

Zawadi anasema huyo mwanaume alimtumia ujumbe mfupi kwenye simu unaosomeka“sihusiki na hiyo mimba, mtafute baba wa mtoto.”

Zawadi anasema baada ya kusoma ujumbe ule akachanganyikiwa maana wakati huohuo alichachamaa akaishia kupunguzwa kazini.

Anasema kilichomuuma zaidi ni kwamba kwenye gate la ofisi kulibandikwa tangazo linalosomeka “Kuanzia leo Zawadi si Correspondent wa ofisi hii, haruhusiwi kuingia katika geti hili”.

Zawadi anasema aliamua kurudi kijijini kwao kujifungua na sasa amejutia maisha na ameamua kuanza maisha upya kwa kuanza kujishughulisha na biashara ndogo kuuza chakula

Ushauri wake kwa wasichana

Zawadi anawaasa mabinti wanaomaliza vyuo na kwenda kujitolea kwenye vyombo vya habari au wameaajiriwa wasikubali utendaji wao wa kazi upimwe kwakutokana na wao kukubali rushwa ya ngono.

“Ninajutia sikukataa vishawishi vya wanaume viongozi wangu kazini, sasa natambua nilitenda kosa, natamani siku zirudi nyuma nirekebishe makosa yangu lakini nimeshachelewa acha tu nipambane na hali yangu”, anasema.

Zawadi ni mmoja wa wanawake wachache vijana waandishi wa habari ambao wameamua kuvunja ukimya dhidi ya rushwa ya ngono, Rushwa hii ni kosa la jinai na watu wenye mamlaka kutumia kama ndoano ya kuwanasa wanawake vijana wanapotafuta ajira au haki zao nyingine kwenye sehemu za kazi.

Kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) (2022) matukio ya ukatili wa kingono dhidi ya wanawake na watoto yameongezeka kwa asilimia 80 katika kipindi cha miaka mitano kati ya 2018 na 2022 na mkoa wa Dar esSalama ndio ulikuwa na matukio mengi zaidi.

Ripoti hiyo inaonyesha katika mikoa sita iliyotembelewa kwaajili yaukaguzi mwaka 2022, Dar es Salaam yameripotiwa matukio 1,656 ikilinganishwa na matukio 326 ya mwaka 2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 407.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanawake Wanahabari Tanzania (TAMWA) Dk Rose Reuben amesema mwaka 2021 shirika hilo lilifanya utafiti nakubaini kwamba rushwa ya ngono ipo katika vyombo vya habari nchini.

Hata hivyo “ni asilimia 48 tu yawanahabari walioojiwa ndio walisema kuhusu madhila ya rushwa ya ngono waliyoyapata wakati asilimia 52 walikaa kimya”, anasema na kuongeza;..

“Matokeo ya tafiti na uchapishaji wa habari kuhusu rushwa ya ngono, yalichagiza wadau na waathirika kuweka wazi hali halisi ya rushwa ya ngono na unyanyasaji wa kingono katika mazingira ya kazi na elimu,” anasema na kuongeza.

Rushwa ya ngono ni kosa la jinai na inashughulikiwa kisheria kwa mujibu wa Kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/ 2007.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili wa kijinsia (MKUKI) Wakili Anna Kulaya anasema ”wapo viongozi katika maeneo ya kazi, wanaotoa kazi kwa upendeleo kwa kuomba rushwa ya ngono badala ya kuangalia uwezo na vipaji vya mtu.”

Amesema kila mtu anapaswa kupinga vita rushwa ya ngono vyuoni na mahali pa kazi na ameiomba Serikali kuharakisha kuridhia mkataba wa C190, hii itasaidia kutokomeza Rushwa ya Ngono na Unyanyasaji mahala pa kazi ifikapo 2030.

Mwakilishi wa Mtandao wa Ushirikishaji Wanaume ‘Men Engage’ (MET) Dk. Katanta Simwanza anasema katika kupambana na rushwa ya ngono ni muhimu wanaume wahusike kikamilifu.

“Wanaume tujuwe rushwa ya ngono inaua ndoto za wanawake wengi, tujikite kukagua ujuzi wa mtu kitaaluma na utendaji wake na siyo maumbile ya mwili,” anasema Simwanza.

Rayna Eben, msichana anayefanya kazi benki moja jijini Dar es Salaam, anasema “wakati mwingine sisi wasichana tuna katabia ya kutaka feva za hapa na pale siyo vizuri zinachochea rushwa.

Anasema“ni vema sisi wasichana tujithamini, tuzingatie kuwajibika maana kama mwanamme mwenye madaraka kazini kwako atataka kukurudisha nyuma kwa kumkatalia rushwa ya ngono, kama utendaji wako ni mzuri itakuwa ni vigumu kukukwamisha maana kazi yako nzuri itazungumza”.

“Nilikua na wakati mgumu sana”

Na Mwandishi Wetu

“Nilikua na wakati mgumu sana kwenye ile ofisini, nikajikuta utendaji wangu wa kazi unashuka, sikua na raha kwasababu waliniumiza sana kiakili”,

Hivi ndivyo Rebecca Sospeter (sio jina lake halisi) mwandishi mwanamake mwenye Shahada ya Pili (Masters’s) kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda anavyoelezea athari ya rushwa ya ngono kwenye maisha yake ya uandishi wahabari.

Anasema “wapo mabosi wanaume walikua hawapendi ile hali, Mmoja wapo ni (anataja jina) yeye ndio alikua akinipamoyo na kuniambia nipambane nisikubali kumpa shetani ushindi”.

Katika mahojiano maalum Rebecca anasema alipata bahati yakuajiriwa kwenye vyombo tofauti vya habari na kwamba kuhama kwake kutoka chombo cha habari kimoja kwenda kingine nikwaajiliya kutafuta penye maslahi bora zaidi.

Hata hivyo, anasema sikama alivyotaraji kwasababu chombo cha Habari cha mwisho alichofanyia kazi alikumbana na vikwazo vingi situkutoka kwa wakubwa zake wa kazi bali pia mpaka kwa wafanyakazi wenzake wa kike kwakile walichodai “anaringa na vingereza vingivingi.”

“Mwanzoni nilipuuza, niliona ni wivu tu, lakini hali ilikua mbaya baada ya bosi wangu wa kiume kunitaka kimapenzi, nilikasirika kwa kuona amenidharau, haniheshimu licha ya kujua Mimi ni mke wa mtu, tena Mume wangu anamfahamu lakini bado akawa ananisumbua kimapenzi,“ anasema Rebecca.

Uk 23



Uk 22

" Nilikuwa na wakati mgumu ...

Anasema, alijikuta anaingia kwenye mgogoro mkali zaidi na bosi wake huyo ambae alikua akimpangia kazi ngumu nakumuhamisha vitengo ilitukumshusha utendaji kazi wake.

Rebbeca anasema hali ile ya unyanyasaji aliyokua akifanyiwa wapo baadhi ya waandishi wenzake wa kike walionekana kuhifurahia na hata kumuwekea vikao vya kumsengenya kwakudai kuwa anaringa.

"Hali ilipokua mbaya ofisini nilimshirikisha Mume wangu, lakini hakua na la kusema ukizingatia nae kwa wakati huo alikua kapoteza kazi baada yakupunguzwa kazini, ilibidi nivumilie, nipambane, maana nikisema niache kazi tuna watoto, tutaishije.

Anasema, mgogoro kati yake na bosi wake ulizidi kuwa mkubwa baada ya yeye kugoma kuburuzwa, hivyo akapewa barua ya kuachishwa kazi.

"Sikukubali maana nilijua ni uonevu, nikaenda mahakama ya kazi, nashukuru nilishinda kesi na kurejeshwa kazini nastahiki zangu zote nikapatiwa." Anasema na kuongeza

"Lakini pamoja na yote nikawa sipewi ushirikiano wa aina yoyote, nikifika asubuhi na sign basi nakaa nasoma magazeti, muda wakutoka ofisini natoka.

"Hali ile ilinichosha, maana nilijikuta napokea mshahara ambao sijautumikia, nikatafuta kazi taasisi ya serikali, ndiko nilipo hadi leo katika kitengo cha Mawasiliano kwa Umma, changamoto zipo ila napambana."Anasema

Akizungumzia masuala ya rushwa ya ngono makazini, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk Dorothy Gwajima anasema rushwa ya ngono ni ukatili kama ulivyo ukatili mwingine.

Waziri Dkt. Gwajima anasema rushwa ya ngono inachangia migogoro kazini, hofu, afya ya akili na changamoto ya madhara ya kiuchumi.

Anaongeza, "inapunguza nguvu kazi ya taifa, kuleta umaskini na kusababisha jamii kuishi kwa hofu,"

Aidha, anasema katika kipindi cha kuanzia Januari, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya matukio ya ukatili 15,901 yaliripotiwa Polisi.

"Mathalani katika matukio haya ni mashauri 671 tu ndiyo yaliyofikishwa mahakamani ambapo kati yake mashauri 368 yalizotolewa hukumu na 303 bado kesi zake zinaendelea," amesema Waziri Dkt Gwajima.

Amesema, sehemu kubwa ya jamii imekuwa haionyeshi ushirikiano wakutosha kwenye kutoa ushahidi ili kesi itayarishwe vizuri kukidhi vigezo vya kufikishwa mahakamani hali inayoathiri upatikanaji wa haki.

Mtaalamu wa Masuala ya Jinsia, Afya, uzazi, familia na malezi Dkt. Katanta Simwanza akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tatizo la rushwa ya ngono katika vyumba vya habari.

Akizungumzia suala la rushwa ya ngono Mkurugenzi wa Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA), Tike Mwambipile anasema sheria ya ajira na mahusiano kazini namba 6 ya mwaka 2004 inataka watu wakiwa sehemu za kazi kuhakikisha kufanya kazi kwa kuheshimu utu

Amesema sheria hiyo pia inapinga ukatili sehemu za kazi naamewataka watumishi wote nchini kutofumbia macho vitendo vya kikatili.

Vile vile Mwambipike anasema Kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/ 2007 nacho kinapiga vita rushwa ya ngono.

Amefafanua kwamba kifungu hicho kinasema mtu yeyote ambaye kwa kutumia nafasi yake au mamlaka yake katika kutekeleza majukumu yake anaomba au kutoa upendeleo wa kingono au upendeleo mwingine wowote kama kigezo cha kutoa ajira, kupandishwa cheo, kutoa haki au upendeleo wowote unaotambulika kisheria, atakuwa ametenda kosa chini ya kifungu hiki.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake nchini (TAMWA), Dkt Rose Reuben amesema rushwa ya ngono mahala pa kazini siyo tu niukatili ambao unamvuruga mtu kisaikolojia bali pia ni chanzo cha kushuka kwa uzalishaji na kuenea kwa virusi vya HIV vinavyosababisha UKIMWI.

Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira anasema rushwa ya ngono ni ukatili wa jinsia unaopaswa kupingwa na makundi ya aina yote na maeneo yote nchini.

Rehema Maro afisa kutoka shirika la wanawake na la Sheria na MaendeleoAfrika (WILDAF) tawi la Tanzania anasema "ukatili unaotokea maeneo ya kazi hauathiri ofisi tu unakwenda hadi kwenye ngazi ya familia."

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari za Mtandaoni, kutoka Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) Sylvester Domasa anasema sehemu za kazi inapaswa kuwa ni sehemu salama vinginevyo morali ya kazi inapotea... hivyo sote tuchukue hatua kukomesha rushwa ya ngono ."

Usiri unaendeleza rushwa ya ngono

Na Penina Malundo

Wanawake wengi nchini hukabiliwa na changamoto ya kuombwa rushwa ya ngono na watu wenye mamlaka vyuoni na sehemu za kazi lakini badala ya kuwachukulia watu hao hatua za kisheria, huamua kukaa kimya.

Amina Saidi (sio jina lake halisi) mwenye umri wa miaka 27 ni Mmoja wa waandishi wa habari wanawake ambao wameomba rushwa ya ngono, wakakataa lakini wakakaa kimya bila kuchukua hatua.

Amina anasema alipokuwa chuoni akisomea uandishi wahabari alitakiwa kwenda kutafuta nafasi yakufanya mafunzo kwa vitendo na alifanikiwa kupata nafasi katika chombo kimoja cha habari.

Anasema muda wote akiwa katika chombo hicho cha habari alikuwa anasumbuliwa na Mhariri wake kwa kumtaka afanye naye mapenzi lakini hakumkubalia na hilo jambo alibaki nalo likimuumiza bila kumueleza mtu yeyote wala kumchukulia hatua huyo mhariri wake.

“Sikumweleza mtu yeyote kwasababu niliona nikimwambia mtu yeyote halafu ikasambaa na kumfikia Mhariri wangu nitajiharibia masomo yangu kwa vitendo”, anasema Amina.

Amina anasema akiwa anamalizia masomo mwaka wa pili, alipata taarifa kuwa chombo kile cha habari alichofanya masomo kwa vitendo walikuwa wanatafuta watu wakujitolea na yeye aliomba kwenda kujitolea. » Uk 25

Uk 24

Usiri unaendeleza rushwa ...

“Yule mhariri niliyemkatalia urafiki wa mapenzi ndiye aliyekuwa anapokea watu wakujitolea na nilimuomba nafasi akakataa, nikaondoka kwenda kutafakari”, anasema Amina.

Anasema baadaye “niliamua kuacha kufikiria kabisa kwamba kazi ya uandishi wa habari itanisaidia maisha yangu badala yake nikaamua kufungua biashara zangu na nimezifanya tangu nimemaliza chuo mwaka 2019 hadi sasa”.

Mwanahabari mwingine mwanamke Atonia John (sio jina halisi) anasema alikuwa anajitolea kwenye gazeti fulani lakini mwaka jana (2022) meneja wa radio moja mkoani Dar es Salaam alimkaribisha kufanya kazi katika radio hiyo lakini baadae akaanza kumwambia ampe rushwa ya ngono ili aweze kupata kazi kwenye ofisi hiyo.

Anasema baada ya kusikia hivyo aliamua kwamba ni bora kubaki katika kituo chake cha awali akijitolea kuliko kutoa mwili wake kwa ajili ya kazi ambayo nayo hana uhakika nayo. Hata hivyo naye alikaa kimya hakuchukua hatua yoyote.

Wanaoombwa rushwa ya ngono kuendelea kukaa kimya kumekuwa na madhara kwasababu wanaoomba rushwa hiyo wamekuwa wakiendeleza tabia hiyo kwakudhani kwamba hakuna chochote kinachoweza kufanyika dhidi yao. Matokeo yake wanawake wengi waandishi wa habari wamejikuta wakiombwa rushwa ya ngono.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Dk Rose Reuben anasema shirika hili lilifanya utafiti Dar es Salaam ambapo asilimia 48 ya waandishi wa habari wasio na ajira rasmi walisema wamewahiombwa rushwa ya ngono katika vyombo vya habari.

Lakini cha kusikitisha ni kwamba, ingawa kuna sheria rasmi inayosema wazi kwamba rushwa ya ngono ni kosa la jinai, waandishi hao wanawake waliopitia madhila ya rushwa ya ngono hawakuchukua hatua za kisheria.

Hata hivyo wakati wa utafiti huo wanawake waandishi wa habari waliofikiwa nakutakiwa kuzungumzia rushwa ya ngono hawakutaka kusema lolote kama anavyodokeza Dk Rose “asilimia 52 walikaa kimya; hawakuwa tayari kusema kuhusu rushwa hii… nasisitiza hii ni kwa wachache tuliowafikia.”

Kwa mujibu wakifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 mtu anayebainika kutumia mamlaka ya utekelezaji majukumu yake kuomba au kutoa upendeleo wa kingono, kama kigezo cha kutoa ajira, kupandisha cheo, kutoa haki au huduma, atashitakiwa chini ya Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi.

Sheria hiyo inasema mtu akitiwa hatiani kwa kosa la rushwa ya ngono, anaweza kuhukumiwa faini isiyozidi Sh milioni tano, au kifungo cha miaka 20 jela, au adhabu zote kwa pamoja.

Kwahiyo, ni vema kila mwanamke wa Tanzania na hasa mwandishi wa habari anapokuwa chuoni au anafanya kazi kwenye vyombo vya habari kwa mafunzo au kujitolea au ameajiriwa atambue kwamba hapaswi kukaa kimya inapotokea mwanaume mwenye mamlaka kumuomba rushwa ya ngono. Ni lazima achukue hatua ili mwanaume huyo atambue rushwa ya ngono ni kosa la jinai.

Mapambano dhidi ya rushwa ya ngono ndani ya vyombo vya habari

Warsha ya waandishi wa habari wanawake na wabobezi wa habari. Mkoa wa Dar es Salaam

Mafunzo kwa wahariri, wamiliki wa vyombo vya habari, mameneja, na wanahabari wanawake, Mkoa wa Dar Es Salaam.

Mijadala mbalimbali iliyoendeshwa na TAMWA kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya kijinsia, Serikali na vyombo vya habari katika harakati za kupinga rushwa ya ngono ndani ya vyombo vya habari.

Majadiliano na wanahabari wanaume, Mkoa wa Dar es Salaam.

Mdahalo wa wahariri, wamiliki wa vyombo vya habari, mameneja, na wanahabari wanawake, Mkoa wa Dar es Salaam.

Rai yangu kwa Wanawake ndani ya vyombo vya habari waweze kupata ushahidi uliokuwa mzuri wa masuala haya ya rushwa ya ngono angalau wapate vitendo vya awali vya ushawishi na kutoa taarifa katika madawati yao ya kijinsia ili sisi tuweze kupata taarifa hizo na kukamilisha ushahidi huo, kuufanyia mitego na kufikisha kesi mahakamani. Bibie Mssumi, Mkuu wa Dawati la Elimu Kwa Umma, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU Kinondoni)